Liberté • Égalité • Fraternité
RÉPUBLIQUE FRANÇAISE

MINISTÈRE
DE L'EUROPE ET DES
AFFAIRES ÉTRANGÈRES

DIRECTION GÉNÉRALE DE L'ADMINISTRATION
ET DE LA MODERNISATION

DIRECTION DES RESSOURCES HUMAINES

Sous-direction de la Formation et des Concours

Bureau des Concours et Examens professionnels
RH4B

CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCÈS A L'EMPLOI DE SECRETAIRE DES AFFAIRES ETRANGÈRES (CADRE D'ORIENT) AU TITRE DE L'ANNÉE 2020

ÉPREUVES ÉCRITES D'ADMISSIBILITÉ

Jeudi 19 septembre 2019

SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures
Coefficient : 2
Toute note inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire.
Barème de notation : composition en swahili 12 points ; traduction en français 8 points

COMPOSITION EN SWAHILI

Composition en swahili à partir d'une question, rédigée dans cette même langue, liée à l'actualité.
(350 mots avec une tolérance de plus ou moins 10%)

SUJET :

« Uhamiaji unaathirije maendeleo ya bara la Afrika upande wa kisiasa, kiuchumi na kijamii ? »

Liberté • Égalité • Fraternité
RÉPUBLIQUE FRANÇAISE

MINISTÈRE
DE L'EUROPE ET DES
AFFAIRES ÉTRANGÈRES

DIRECTION GÉNÉRALE DE L'ADMINISTRATION
ET DE LA MODERNISATION

DIRECTION DES RESSOURCES HUMAINES

Sous-direction de la Formation et des Concours

Bureau des Concours et Examens professionnels
RH4B

CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCÈS A L'EMPLOI DE SECRETAIRE DES AFFAIRES ETRANGÈRES (CADRE D'ORIENT) AU TITRE DE L'ANNÉE 2020

ÉPREUVES ÉCRITES D'ADMISSIBILITÉ

Jeudi 19 septembre 2019

SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures
Coefficient : 2
Toute note inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire.
Barème de notation : composition en swahili 12 points ; traduction en français 8 points

TRADUCTION EN FRANÇAIS

Traduction en français d'un texte rédigé en swahili.

TEXTE AU VERSO

Note : Les deux textes sont à traduire

Pars Today, 08/06/ 2019

Wapinzani Sudan wakubali kwa masharti Ethiopia kuwa mpatanishi

Kwa mujiibu wa taarifa, Jumuiya ya Wanataaluma Sudan (SPA) ambayo imekuwa mstari wa mbele kuongoza maandamano ya wananchi, siku ya Ijumaa ilitoa taarifa na kusema inaafiki upatanishi usio wa moja kwa moja wa Ethiopia na kusisitiza kuwa upatanishi wowote unapaswa kufanyika kwa lengo la kutekeleza mpango wa jeshi kuwakabidhi raia madaraka. Aidha jumuiya hiyo imetahadharisha kuhusu njama ya Baraza la Kijeshi la Mpito kutumia mamluki na wahuni kueneza fujo na kuwashambulia wapinzani katika maeneo mbali mbali ya mji mkuu Khartoum.
Abiy Ahmad Ali, Waziri Mkuu wa Ethiopia jana ijumaa alifika mjini Khartoum na kukutana na mkuu wa Baraza la Kijeshi la Mpito Abdel Fattah Abdelrahman Burhan na ujumbe wa makundi ya wapinzani. Waziri Mkuu wa Ethiopia ametahadharisha kuhusu uingiliaji wa madola ya kigeni katika mambo ya ndani ya Sudan.
Wakati huo huo tovuti ya Middle East Eye imesema kwamba, Kiongozi wa Baraza la Kijeshi la Mpito huko Sudan Jenerali Abdel Fattah al Burhan aliidhinishwa na Saudi Arabia na waitifaki wake kufanya mashambulizi dhidi ya raia waliokuwa wamekusanyika na kufanya mgomo mbele ya makao makuu ya jeshi la nchi hiyo Jumatatu iliyopita ambalo liliua zaidi ya raia mia moja. […].

Nombre de mots : 196

Pars Today, 25/06/2019

UN yalitaka jeshi la Sudan liache kukandamiza wananchi

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, Michelle Bachelet alitoa mwito huo jana wakati wa kikao cha ufunguzi cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa mjini Geneva Uswisi na kuongeza kuwa, wanajeshi nchini Sudan wanapaswa kuacha kukandamiza maandamano ya wananchi na wawafungulie wananchi hao mawasiliano ya Intaneti.
Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa ameongeza kuwa, ofisi ya Kamisheni ya Haki za Binadamu ya umoja huo imepokea ripoti nyingi zinazoonesha kuwa zaidi ya raia 100 wa Sudan waliuawa tarehe 3 mwezi huu wa Juni mbele ya Wizara ya Ulinzi mjini Khartoum na mamia ya wananchi wengine hawajulikani walipo hadi hivi sasa.
Aidha Bachelet amelitaka jeshi la Sudan liruhusu wachunguzi wa kimataifa waingie nchini humo kufanya uchunguzi juu ya mauaji hayo ya umati. Hata hivyo majenerali wa kijeshi wa Sudan wamepinga mwito huo.

Nombre de mots : 147,

Total des deux textes : 343 mots